

HALMASHAURI YA WILAYA MPANDA



Simu: 025 - 2820068
Fax No. 025-2820068
E-mail: ded@mpandadc.go.tz
Website: www.mpandadc.go.tz
Kumb Na. KTV/MDC/D.10/1056/01

**S.L.P 1
MPANDA**

28/8/2018

MWALIKO WA UWEKEZAJI

UWEKEZAJI WA UJENZI WA VIBANDA KATIKA MAENEO YA VITUO VYA MAGARI (BUS STAND) LUHAFWE, KASEKESE, MAJALILA NA IKOLA

Halmashauri ya Wilaya Mpanda inapenda kuwaalika watu binafsi, makampuni, ushirika, taasisi au vikundi vya watu wenye nia, uwezo na uzoefu wa kuwekeza katika kujenga vibanda/maduka kuzunguka maeneo yaliyopimwa na kutengwa kwa ajili ya vituo vya mabasi (Bus Stand Shops). Wananchi wote wanaalikwa kutuma maombi yao ya uwekezaji katika maeneo ya Luhafwe, Majalila (Makao makuu), Kasekese na Ikola kwani Halmashauri imetenga maeneo hayo kwa kuyapima na kuyapatia Hati kwa lengo la kuweka mazingira rafiki ya kufanikisha lengo la kuendeleza miji hii inayokuwa kwa kasi.

1. Maombi yote ya uwekezaji yazingatie masharti yafuatayo:
 - a) Nyaraka za uwekezaji zitapatikana kwa kulipia ada ya **Tshs 50,000/= (elfu hamsini tu)** ambayo haitarudishwa. Malipo yanapaswa kufanywa kwa kulipia Benki **NMB** akaunti ya Halmashauri yenye jina la **OWN SOURCE COLLECTION** akaunti namba **61910000767**, na kuleta "bank pay in slip" kwa ajili ya kukatiwa stakabadhi ya Halmashauri, mwombaji atatembelea eneo la uwekezaji/ujenzi wa vibanda/maduka kabla ya kuchukua nyaraka za uwekezaji ambazo zitatolewa baada ya kutembelea eneo la kituo cha magari husika. Kutembelea eneo la uwekezaji (Bus stand) litagharimiwa na mwombaji mwenyewe;
 - b) Ombi la uwekezaji liwe na majina na anuani halisi ya mwombaji;
 - c) Mwombaji awe na uwezo wa kujenga kibanda/maduka chote pamoja na miundombinu yote muhimu kwa muda wa miezi mitatu akizingatia ubora, maelekezo na michoro iliyotolewa na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mpanda;
 - d) Mwombaji awe na uwezo wa kujenga majengo hayo kwa gharama zake na ukokotoaji utafanyika ili kupata gharama halisi za ujenzi na mkataba

- utaainisha namna ya kurejesha gharama hizo katika kipindi Fulani kabla ya ujenzi kuanza ili kuweka misingi imara ya kuendeleza maeneo husika;
- e) Zingatia kuwa fomu ya maombi ya uwekezaji inajazwa kikamilifu, kusainiwa na kuwasilishwa na mwombaji wa uwekezaji mwenyewe. Iwapo kutokana na sababu za msingi mwombaji atashindwa kutekeleza jukumu hili basi ateue mwakilishi mwenye nguvu ya kisheria "power of attorney" kufanya kazi hiyo;
2. Mwombaji anatakiwa kulipa kiasi cha **Tsh. 100,000/= (Laki moja tu)** kama **Amana** ya Uwekezaji (**Bid Security**) kwa kulipia Benki akaunti ya amana ya Halmashauri "**MDC MISCELLANEOUS DEPOSIT**" akaunti namba **61910000771**, na kuleta "bank pay in slip" Kwa ajili ya kukatiwa stakabadhi ya Halmashauri ambayo itarudishwa baada ya mchakato wa uwekezaji kukamilika. Endapo mwombaji akijitoa kabla ya mchakato wa uwekezaji haujakamilika hatarudishiwa fedha husika;
 3. Mwombaji awasilishe nyaraka halisi za uwekezaji (**Original**) na **nakala 3 [tatu]** zilizotimia vyema na kusainiwa kurasa zote;
 4. Nyaraka za uwekezaji zijazwe vizuri, ziwekwe kwenye bahasha ifungwe vyema na juu ya bahasha iandikwe, anuani kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni, S.L.P 01, Mpanda.
 5. Halmashauri hailazimiki kupitisha uwekezaji wowote isipokuwa uwekezaji uliokizi vigezo;
 6. Mwisho wa kupokea nyaraka za uwekezaji ni tarehe 28/09/2018 saa nne (4.00) kamili asubuhi katika ofisi za **Halmashauri ya Wilaya, S.L.P 1, Kitengo cha Manunuzi na Ugavi**;
 7. Nyaraka za uwekezaji ambazo zitacheleweshwa kwa muda uliopangwa na nyaraka za kielekitroniki (e-mail) hazitapokelewa.



Samson Z. Medda

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA MPANDA**

**MKURUGENZI MTENDAJI CWD
MPANDA**